

Pambazuko

Toleo Namba 050

Jumatatu Oktoba 16-22, 2023



Jicho la Tai

**Kikwete kamjulie
hali Lowassa**

Uk. 5



**Israel
VS
Palestina**

**Nani
wanufaika
wa vita?**

**Uk.
11**



**Vilainishi
haviepushi
Ukimwi**

Uk.6

**Wakili ICC
atamani
Katiba
mpya
Tanzania**

Uk.15

**Changia uhai
wa Pambazuko**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

Tahariri**Tunasimama na Palestina**

Tahariri

(Haya mwanachama wa Pambazuko ndani

ya Pambazuko)



WAHENGA WETU



Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kulia), akiwa na aliyewahi kuwa msaidizi wake wa karibu; Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, Jonh Malecela. Picha hii iliyopatikana kwenye mitandao ya jamii, haikuwa na maelezo zaidi ya mahali ilipopigwa na nani alitipiga. Imewekwa hapa kwa ajili ya kumbukumbu tu ya miaka 24 iliyopita tangu kufariki kwa Mwalimu Nyerere.

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Ukitaka kufanikiwa zaidi, tembea, kutana na watu na kikubwa zaidi, zungumza nao. Kamwe usijifungie chumbani na kusubiri neema na heri kutoka popote. Kinyume na haya, utageuka kuwa mtu wa kulalamika na kuona waliofanikiwa kujawa “ushetani.” – Msemo wa Kichina.

Tangazo

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufurahia kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakitumia fedha, muda, ujuzi na rasirimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiswahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokua zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili – miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukuza Kiswahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoa uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majeraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kuimarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili lianze kuuzwa, lakini haukubaliani na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapenda kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako

na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya “asante” kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi – kwenda namba hii ya Lipa kwa TiGO na utatufikia; 6214500

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: Pambazuko Gazeti.

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako – na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

*Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023*

JK nenda kamsabahi Lowassa

Na Igo AI

TAI amekaa muda mrefu akimuomba rafiki yake wa siku nyingi, Edward Ngoyai Lowassa, yule aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, baada ya kuelezwa kwamba amekumbwa na changamoto ya afya kwa muda mrefu sasa.

Hata hivyo, Tai akapiga akili na nafsi ikamsuta kwamba kuomba peke yake hakutoshi na hata kutuma senti za kununua matunda kwa mgonjwa hakutoshi.

Tai akaamua kuruka hadi nyumbani kwa Lowassa, pale Monduli, ili kumjulia hali swahiba wake wa siku nyingi sana. Hakutaka kumpigia simu mke wa Lowassa, Mama Regina wala kumsumbua Fred, kijana wa Lowassa ili kujua hali ya rafiki yake.

Tai aliamini kuwa kwa kuwa Dar es Salaam Lowassa hayupo, lazima atakuwa Monduli, hivyo hakujisumbua. Huyooooo hadi Umasaini.

Ebhanaa eh! Kufika Monduli akaelezwa kwamba swahiba wake hayupo, yuko nje ya nchi akiendelea kwa matibabu.

Tai akajiinamia, akasikitika mno na kujiuliza, kwani hali yake imebadilika kiasi hicho hadi kupelekwa huko nje? Kwani dawa za Masai zimeshindwa. Je, hapo kwa Profesa Janabi napo wamekwama? Shida ni nini?

Hakika maswali haya hayakuwa na majibu, lakini akajipa moyo konde kwamba lazima aruke hadi alipo Lowassa wake amjulie hali na kuona maendeleo ya afya yake ndipo moyo na roho yake "vitapoa."

Tai hakuwa na muda wa kupoteza, huyooooo hadi kwa Mandela, kule Bondeni, akaelekezwa na Fred alipo mzee wake.

Kufika tu, pamoja na kumkuta rafiki yake anaendelea vyema, lakini alishuhudia bashasha la salamu la kawaida la Lowassa siyo lile "orjino."



Lowassa akiwa na JK

Tai akakaa kwa muda akijipa moyo kwamba Mungu ni mwema, atatenda maajabu yake ili swahiba wake huyo arejee nyumbani akiwa buheri wa afya.

Tena akaamani arudi naye nyumbani aendelee kufurahia uwepo wa wajukuu zake na marafiki wengine ambao walizoea kumtembelea nyumbani mzee wake huyo.

Kabla ya kubaini matamano yake kurejea na Lowassa nyumbani ni madogo, Tai akaamua kuuliza endapo rafiki yake mwingine, ambaye pamoja naye, ni marafiki wakubwa wa Lowassa, kama amefika kamsabahi.

Akaambiwa kwamba swahiba wake mwingine, kwa jina la Jakaya Kikwete hajafika kumjulia hali rafiki yao; kwanza akaamini huenda siyo yule JK anayemfahamu. Iweje hajaenda kumjulia hali Lowassa.

Tai akaikumbuka ringi ya urafiki wa Lowassa na Kikwete. Akakumbuka "sarakasi" za wawili hao kugombea uongozi wa juu wa Tanzania. Akaikumbuka "boizitumeni."

Nafsi ikakataa kwamba iweje Kikwete hajaenda kumpa salamu za moja kwa moja swahiba wake?

Haiwezekani! Akajiapiza na kuamua kupiga simu kwa JK kumsihi aende kumjulia hali. Simu haikupatikana na akaamua kufika Pambazuko kupaza zauti.

Wasiliana na mjumbe wa Tai kupitia namna hii: 0744 768 263

Habari

Vilainishi havizuii kuambukizwa Ukimwi

Na Mwandishi WETU

MATAMANIO ya Tanzania ‘kufurusha’ maambukizi mapya ya ugonjwa wa Ukimwi ifikapo mwaka 2023, huenda yakabaki kuwa ndoto, Pambazuko linaeleza kinagaubaga.

Hofu hiyo inatokana na matokeo ya uchunguzi uliofanywa na gazeti hili kwa zaidi ya miezi miwili katika miji ya Dar es Salaam, Mbeya na Bukoba katika kutambua kuimarika kwa njia za kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU (Virusi Vya Ukimwi).

Pambazuko lilitengeneza mfumo-hojaji wa kisasa kwa kutumia simu ya mkononi kukusanya maoni ya wananchi mmoja mmoja, wenye maduka ya dawa, watumishi wa maeneo ya starehe, watumishi wa nyumba za kulala wageni na wanaofanya biashara ya ngono.

Katika hali isiyotarajiwa, matokeo ya uchunguzi huo yameonesha kwamba matumizi ya kondomu yamepungua zaidi, huku wengi wanaojihusisha na ngono wakitumia zaidi vilainishi.

Imebainika kwamba idadi kubwa ya watu wanaojihusisha na “ngono za kununua” wanapendelea zaidi kutumia vilainishi; hasa mafuta ya mgando, mafuta ya nazi ya maji na kutumia jeli.

Takwimu zilizokusanywa, zinaonesha kwamba Dar es Salaam, pamoja na kuwa mkoa wa tatu kwa kuongoza kwa maambukizi ya ugonjwa huo, ikitanguliwa na Mbeya na Iringa, ndiyo kinara kwa watu wake kutumia vilainishi kwenye “ngono nzembe.”

Kwamba watu 121 waliohojiwa na Pambazuko katika Jiji la Dar es Salaam lenye watu wanaokadiriwa kuwa zaidi ya milioni tano, wengi walieleza kutopenda kutumia kondomu na sasa wamejielekeza kwenye vilainishi.

Mmoja wa waliohojiwa, mkazi wa Buguruni, Dar es Salaam, alisema kwa kifupi na haraka-haraka kwamba “Ukimwi



Wasiri wa Afya - Umy Mwalimu

kwa sasa hauogopeshi, hivyo ni mwendo wa kula raha.”

Katika zoezi hilo la Pambazuko, wengi waliohojiwa walikuwa wanaume – wenye umri kati ya miaka 19 hadi 42, ambao walionesha ushirikiano mkubwa na kuwa huru zaidi kuzungumza kuliko wanawake, ingawa Bukoba hali ilikuwa tofauti.

Dar es Salaam waliohojiwa watu 121 (wanawake 32); Mbeya 67 (wanawake 13) na Bukoba 82 (wanawake 54).

Katika miji hiyo, Pambazuko lilitembelea maduka kadhaa ya dawa baridi na kubaini kwamba ununuzi wa kondomu, au maarufu kwa jina la “zana,” umepungua kwa kiasi kikubwa.

Katika maduka yaliyotembelewa jijini Mbeya, watendaji wengi wa maduka hayo walikuwa wakijibu kwamba “kondomu kwa sasa hazitoki sana.” Walipoulizwa sababu, walieleza kwamba “huenda watu wamekuwa waaminifu zaidi ama wameacha kufanya mapenzi.”

Hata hivyo, walipoulizwa watu katika maeneo ya starehe katika mji huo, wengi walieleza kwamba watu wengi hawapendi kutumia zana kujikinga dhidi ya maambukizi hayo ya virusi vya Ukimwi.

Wahudumu wa sehemu za kulala wageni katika Mji wa Bukoba, kama ilivyobainika katika maeneo mengi

Vilainishi havizuii kuambukizwa

Inatoka Uk. 6

yaliyofikiwa na Pambazuko, wanaeleza kwamba wanaamini kwamba matumizi ya kondomu yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Wameliambia Pambazuko kwamba miaka mingi iliyopita, walikuwa wakiombwa na wateja wao kupewa kondomu, lakini sasa wanaoziuliza ni wachache.

“Wengi tunawaona wanatuagiza mafuta ya nazi ya maji, na huko tunaamini wanayatumia kwa ajili ya kufanya ngono, wakiamini kuwa ni salama,” anasema mhudumu mmoja wa nyumba ya kulala wageni eneo la Hamgembe.

Pambazuko pia limebaini kwamba kwa wale wasiotumia kondomu ama vilainishi, wamekuwa wakinunua vipimo rahisi vya maambukizi ya Ukimwi na wanapopata majibu ya haraka kwamba mwenzi hajaambukizwa, basi huamua kufanya “kavukavu.”

Daktari aonya

Daktari wa magonjwa wa binadamu, Laurent Masumbuko anaonya watu kujiaminisha kwamba matumizi ya vilainishi sehemu za siri kabla ya kufanya ngono, ni njia sahihi ya kujikinga dhidi ya maambukizi.

Anasema, pamoja na kwamba maambukizi ya Ukimwi hutegemea muunganisho wa chembe za damu kwa mtu aliyearchukiziwa kwenda kwa mwingine, lakini kutumia vilainishi ni upotofu.

Dkt. Masumbuko anayehudumu katika zahanati ya Huruma, Tabata, Dar es Salaam, anaasa watu kuachana na ngono nzembe, kuwa na mpenzi mmoja asiyeambukizwa, na kama kuna ulazima wa kufanya ngono, basi kutumia kondomu kwa usahihi.

Anasema katika kutekeleza tendo la ndoa, upo uwezekano wa kupata michubuko midogo zaidi, ambayo inaweza kuwapa mwana virusi kupenya.

Daktari mwingine wa Hospitali ya Mkoa wa Kagera, anaeleza kwamba katika kupima virusi, kuna wakati haviwezi kuonekana kwa kupima mara moja, na hasa kama mwenza mmoja ameanza kutumia dawa za kurefusha maisha.

Huku akikataa kutaja jina lake gazetini, anasema watu wengi wanaotumia dawa za kurefusha maisha baada ya kuambukizwa, wakipimwa virusi havionekani haraka, lakini bado wanaweza kuambukiza, hivyo – “watu wawe makini.”

Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids) inaeleza kuwa nchi hiyo imepungua maambukizi ya Ukimwi kwa asilimia themanini na nane kutokana na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kupungua kwa asilimia hamsini (50%) kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka 2020.

Mkurugenzi wa Ufutiliaji na Tathmini wa Tacaids, Dkt. Jerome Kamwela, anasema tafiti zinaonesha kuwa maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima miaka 15 na zaidi yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020 na maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia 7 mwaka 2020.

Dkt. Kamwela anasema kuwa serikali inatakiwa kuongeza nguvu katika eneo la kuzuia maambukizi mapya ya VVU hasa kwa vijana kwani zaidi ya theluthi moja ya maambukizi mapya hutokea kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24, hususan vijana wa kike.

Aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Afya Tanzania, Dkt. Faustine Ndogulile ameshauri kuwepo haja kuwekeza nguvu katika matumizi ya teknolojia kwa kuitumia mifumo ili kurahisisha ufuatiliaji wa matumizi ya dawa za ARV.

Chimbuko la ugonjwa wa Ukimwi liligundukika nchini Tanzania mwaka 1983 ambapo mgonjwa wa kwanza alipatikana katika Mkoa wa Kagera.

Tangazo

Ukiwa Bukoba...

Furahia Nene Freshi Juisi

Pata juisi (sharubati) ya matunda halisi iliyoandaliwa kwa usafi wa hali ya juu kwa kujali afya ya mteja.

Kunywa juisi ya:

Embe	Nanasi/pinacolada
Passion	Tende
Parachichi	Tikiti
Karoti	

Pia tunandaa juisi mchanganyiko maalum wa matunda ili kuondoa uchovu na magonjwa nyemelezi (detox) na pia smoothie.

Waziliana nasi kwa
namba hii:
0753949488





Itifaki ya Rais Samia isifunike kombe

Na Rashid Mtagaluka

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan zaliyoifanya Septemba mwaka huu mkoa ya Lindi na Mtwara imemalizika huku wachambuzi wa masuala ya siasa na kijamii wakionesha matobo yanayopaswa kuzibwa.

Katika ziara hiyo ya kikazi, Rais Samia aliongozana na baadhi ya mawaziri akiwemo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tamisemi, Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa.

Pamoja na kuweka mawe ya msingi katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye mkoa hiyo, Rais Samia alipata nafasi ya kuzungumza na wananchi katika baadhi ya wilaya za mkoa hiyo.

Katika ziara hiyo, mawaziri hao walipata fursa ya kusikiliza kero za wananchi na walitoa ama maagizo au kupatia ufumbuzi baadhi ya kero hizo.

Silaa alimwelekeza mkuu wake, Mhandisi Anthony Sanga kuwachukulia hatua kali watumishi wanne wa Ardhi mkoani Lindi, akiwemo Kamishina wa Mkoa, Geoffrey Martin baada ya kupata malalamiko ya wananchi kutotendewa haki kwenye utwaaji wa maeneo yao.

Hatua hii ya Waziri Silaa ni kutokana na kilio cha mwanamama Ngavena Bakari alichokiangusha mbele ya Rais Samia wakati akizindua Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi akidai kutotendewa haki.

Kule kilwa Rais Samia alipigwa butwaa alipombwa kushughulikia changamoto za wananchi 438 wa Kilwa Masoko zenye zaidi ya miaka 10, akishangaa kero hizo kuchukua muda mrefu bila ufumbuzi wakati viongozi wapo!

Hapa ndipo penye hoja yangu, pamoja na kumpongeza Rais Samia kwa uungwana wa kupokea kero zote



Rais Samia Suluhu Hassan

zilizowasilishwa kwake na wabunge katika maeneo aliyopita, lakini rais amekosa ladha halisi ya kero hizo.

Hii ni kwa sababu zipo taarifa za uhakika kuwa Septemba 12, 2023 kigogo mmoja wa Mkoa wa Lindi aliwaita wafanyabiashara kuzungumza nao, na akawataka wasithubutu kuhoji chochote kuhusu mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Lindi mbele ya Rais Samia. Na kweli hakuna aliyenyanua mdomo wake kugusia hilo!

Ebu fikiria kama changamoto moja tu ya mama Ngavena aliyoisikia imemsukuma waziri wake wa Ardhi kuchukua hatua baada ya kujiridhisha na uzembe wa viongozi wa mkoa, ingekuwaje iwapo wasaidizi wa rais wangeruhusu awasikilize wananchi walau watatu katika kila eneo?

Bila shaka hii ingemsaidia Rais Samia kuchukua hatua papo kwa hapo kulingana na uzito wa changamoto husika na kumuongezea kukubalika kwa wananchi wake.

Ushauri wangu kwa itifaki waache woga, watoe nafasi kwa rais kusikiliza wananchi wenyewe wanama nini mbele ya kiongozi wao ili hatua zichukuliwe.

Mwandishi anapatikana kwa namba: 0784 438 546 au Email: mtagaluka@gmail.com

Mafanikio**Bunju Women yaibuka kidedea**

Na Mwandishi WETU

KIKUNDI cha Kuwezesha Wajasiriamali Wanawake wa Bunju (BWE), kimeibuka mshindi katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa kinara wa kuinua wanawake kiuchumi.

Zawadi kemkem, ikiwamo cheti na nyingine, zilitolewa kwa kikundi hicho chenye makao yake Bunju, Dar es Salaam Jumamosi iliyopita katika hafla iliyoandaliwa na wadau mbalimbali, wakiongozwa na Kituo cha Televisheni cha Channel 10.

Kiongozi wa shughuli hiyo, Jacqueline Salon akizungumza vigezo vilivyotumika kumpata mshindi, alisema kikundi cha BWE kimeibuka mshindi kwa kubainika kwamba kimekuwa kikichochea namna ya kuwaondoa wanawake wengi zaidi katika umasikini.

Amesema, baada ya kushindanishwa na vikundi vingine vya Dar es Salaam, BWE kilionekana kuwa na idadi kubwa ya wanachama wake ambao ni wajasiriamali walioamua kuwa wabunifu wa biashara; ndogo na kubwa na kwamba kwa muda mfupi wanachama wake wengi wamepiga hatua za kiuchumi.

“Uchunguzi wetu, baada ya kupitia vikundi mbalimbali, ukabaini kuwa BWE ilistahili kuwa washindi na hivyo tunawapongeza sana na kuomba wanawake wengine waende Bunju kujifunza kwao,” alisema.

Amesema mafanikio ya wanawake wa Bunju, na hasa wale wanachama wa BWE yako dhahiri, kwani wengi waliohojiwa walieleza kunufaika kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa kundi hilo, kwamba walianza wakiwa na mitaji midogo, lakini sasa kwa kuwa na soko la uhakika, wameongeza mitaji yao.

Akizungumza baada ya kutangazwa washindi, mwenyekiti wa BWE, Jacqueline Mkina aliwashukuru waandaaji na wadhamini wa shughuli hiyo na kwamba ushirikiano wa wanawake wajasiriamali



Baadhi ya wanachama wa BWE wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kutangazwa washindi wa kundi bora la wajasiriamali wanawake Dar es Salaam. Wanaume katika picha hii, ni baadhi ya waandaaji. (Picha kwa hisani ya BWE)

wa Bunju, ndiyo siri ya mafanikio yao.

Jacqueline alisema kikundi chao chenye wanachama wanaokaribia 400, kilianza wakiwa wachache, lakini sasa idadi inaongezeka kila siku, huku bidhaa zinazouzwa zikiongezeka pia.

Alisema mhimili wa kikundi chao, ambacho kilianzishwa ili kusaidia biashara kwa wakazi wa Bunju na maeneo mengine ni; “Nunua Bunju, Uza Popote” umesaidia kuwainua wanawake wengi waliokuwa ama na biashara ndogo zaidi au kutokuwa nazo kabisa.

“Hivi sasa hakuna bidhaa ama huduma zinazokosekana Bunju, tena kutoka kwa wanachama wetu, kila kitu kipo, na mnunuzi siyo lazima awe mwanacha; wote ni wateja wetu bila kujali jinsia wala eneo,” aliongeza mwenyekiti huyo.

Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa mipango ya baadaye ya kikundi hicho ni kuwekeza mtaji mkubwa zaidi wa pamoja ambao utawezesha kuwepo biashara kubwa zaidi, hivyo kujihakikishia mapato makubwa kwa wanachama wake.

“Tumeanza kujadili namna ya kuwa na kitu kikubwa zaidi, huku hizi biashara za mwanachama binafsi zikiendelea, ameongeza.

Alisema pamoja na kufanya biashara, pia kikundi chao kipo kwa ajili ya kusaidiana katika shughuli mbalimbali, kupeana mbinu za biashara na mambo mengine ya kijamii.

Nani mnufaika: Israel vs Palestina?

Na Mwandishi WETU

HALI bado ni tete; ni ya hatari kubwa na huenda kukatokea vifo vingi zaidi vya binadamu na miundombinu kuharibiwa baada ya Kundi la Wanamgambo wa Palestina Islamic Jihad (PIJ) kujiunga na Hamas “kuimaliza Israel.”

PIJ imeamua kujiunga na Hamas ili kuwa na kundi kubwa la Palestina kuishambulia Israel, ikiwa ni njia iliyoitajwa na kundi hilo kuwa ni kulipa kisasi dhidi ya mashambulizi.

Jana Jumapili, Katibu Mkuu wa PIJ, Ziad al-Nakhalah, alisema kuwa kundi hilo linawashikilia Waisraeli 30 na kutangaza kwamba hawataachiwa hadi wafungwa wa Palestina watakapoachiwa kutoka mikononi mwa Israel.

Wakati Palestina inaongeza nguvu, Baraza la Mawaziri la Israel nalo limetangaza “hali ya hatari” baada ya kudai itajibu mapigo kwa mashambulizi makubwa ya kushtukiza yaliyoanzishwa na Hamas.

Taarifa zinaeleza kuwa hadi sasa mapigano hayo yamewaua watu takriban 700 nchini Israel, huku mashambulizi ya anga ya “kulipiza kisasi ya Israel” yakia watu karibu zaidi ya 1000 huko Gaza.

Jeshi la Israel limeendelea na mashambulizi yake makubwa ya anga katika maeneo Gaza jana wakati ambapo wanamgambo wa Hamas wanaendelea kupigana na wanajeshi wa Israel katika maeneo ndani ya mipaka ya Israel.

Wanamgambo wa Hamas walikuwa wakiendelea kudhibiti jamii kadhaa za makazi Kusini mwa Israel Jumapili jioni, huku wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) wakipambana nao kwa risasi.

Swali moja la kujuliza ni kwamba, nani anafaidika kuwepo kwa vita hivyo, vivyoioisha?

Inadaiwa kwamba Russia inayoongozwa na Vladimir Putin ina uhusiano wa karibu na Hamas na kwamba kuthibitisha hilo, Pambazuko



Wapalestina wakibeba miili ya wenzao waliouawa kwa makombora ya Israel.

inazo taarifa kwamba kiongozi wake alitembelea Moscow mwezi Julai, mwaka huu. Putin pia yuko karibu na uongozi wa Iran, ambao wanaunga mkono Hamas na Hezbollah.

Inaelezwa kuwa Putin huenda ndiye muuzaji wa silaha katika vita hivyo, akisaidia Palestina kwa ushirika na swahiba wake, Iran.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Iran ni miongoni mwa wafadhili wakuu wa Hamas.

Kwamba Iran ndiye anaweza kuwa msambazaji wa vifaa vya kijeshi vinavyohitajika haraka, haswa ndege zisizo na rubani.

Inadaiwa pia kwamba huenda Marekani nayo ni mnufaika wa vita hivyo, kwani hata aliyewahi kuwa rais wa nchi hiyo tajiri zaidi duniani, Donald Trump anaeleza hivyo.

Trump tayari anamtuhamu Rais wa Marekani, Joe Biden kwa kuwa na “mikono ya damu” kwenye mauaji hayo yanayoendelea kwenye vita vya Palestina na Israel.

Katika hatua nyingine, baadhi ya wachambuzi wa kimataifa wanadai kwamba tajiri nambari moja duniani, Elon Musk, naye huenda ni mnufaika kwa madai kwamba “anasambaza habari za uongo, kuitetea Palestina.” Tayari Musk amekanusha.

Habari

Tasac yaibua fursa kwa Watanzania

Na Mwandishi WETU

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (Tasac) limeibua maeneo ya uwekezaji ambayo hajayaonekana kwa watu wengi.

Mkurugenzi Mkuu wa Tasac, Nelson Mlali, ameliambia Pambazuko kwamba Tanzania imebeba fursa nyingi za uchumi wa bahari na maziwa, lakini hazikulikana kwa watu wengi.

“Wakati ni sasa kwa Watanzania na watu wengine, kuangalia fursa hizo kwani uwekezaji katika maeneo hayo utasaidia kufungua uchumi wa bluu kwa kiasi kikubwa,” ameegeza.

Moja kati ya fursa hizo zilizojificha ni biashara ya usafirishaji kwa njia ya bahari kati ya Tanzania na visiwa Comoro.

“Comoro ni nchi ya kisiwa ambayo inategemea kila kitu kutoka nje. Ukaribu wake na Tanzania unatufanya tuwe katika nafasi kubwa ya kuwa mhimili wa biashara ya nje ya Comoro, lakini cha kustaaajibisha ni kuwa hakuna usafiri wa uhakika kwa njia ya bahari kati ya nchi hizi mbili...

...Matokeo yake, bidhaa za Tanzania zinazosafirishwa kwenda Comoro ni chache sana,” alisema.

Mlali alibainisha kuwa iwapo kutakuwa na usafiri wa uhakika kwa njia ya bahari kati ya nchi hizo mbili, kiwango cha bidhaa za Tanzania zinazouzwa Comoro kitaongezeka kwa kiasi kikubwa na hilo litawanufaisha sana wafanyabiashara na wazalishaji nchini.

Tasac imeweza kubaini fursa hii kwa sababu majukumu yake makuu ni kuratibu kadhia na shehena inayoingizwa nchini au kusafirishwa nje ya nchi kwa njia ya meli.

Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa ingawa usafirishaji wa bidhaa kati ya nchi hizo mbili unakua kila mwaka, lakini usafirishaji wa huduma kati yake ni kama



Nelson Mlali

vile umedumaa.

Mathalan, wakati mwaka 2021 Tanzania ilisafirisha kwenda Comoro bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 8.75, lakini hakukuwa na huduma zozote zilizopelekwa Comoro mwaka huo kama ambavyo Comoro haikutoa huduma zozote kwa Tanzania, licha ya kusafirisha bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni moja.

Taarifa hizo zinaonesha kuwa bidhaa ambayo ilisafirishwa kwa wingi kutoka Tanzania kwenda Comoro ni saruji (dola 97,000), magodoro (dola 706,000) na maji (dola 598,000).

Katika kipindi cha miaka 26 iliyopita, mauzo ya Tanzania nchini Comoro yameongezeka kwa kasi ya wastani wa asilimia 17.9 kwa mwaka kutoka dola 122,000 mwaka 1995 hadi kufikia dola milioni 8.75 mwaka 2021.

Kwa upande mwingine, bidhaa ambazo Comoro iliuzia Tanzania katika mwaka huo ni pamoja na boti (dola 525,000), injini za boti (dola 393,000), na boti za uvuvi (dola 13,300).

Wakati huohuo, katika kipindi cha miaka 26 iliyopita mauzo ya Comoro nchini Tanzania yameongezeka kwa

Tasac yaibua fursa

Inatoka Uk. 12

wastani wa asilimia 24 kwa mwaka kutoka dola 3,720 mwaka 1995 hado dola milioni moja mwaka 2021.

Uwekezaji ukanda wa pwani

Tasac imebainisha kuwa kuna uwekezaji mdogo sana katika ukanda wa pwani ya Tanzania, hivyo kuacha fursa kubwa ya kiuchumi ikikaa bila kutumika.

Tasac inabainisha kuwa katika ukanda wote wa pwani ya Tanzania; kuanzia Tanga hadi Mtwara, wenye urefu za zaidi ya kilometa 900, hakuna bandari yoyote mahsusi ya uvuvi.

Kwa mujibu wa Mlali, kuna fursa kubwa katika eneo hilo kwa mwekezaji atakayejitokeza kujenga miundombinu itakayosaidia shughuli za uvuvi, ikiwemo bandari za uvuvi, viwanda kwa kuhifadhi na kuchakata samaki na mazao ya bahari.

Mwezi uliopita tu, Septemba Serikali ya Tanzania ilizindua ujenzi wa bandari ya kwanza ya uvuvi inayojengwa wilayani Kilwa, Lindi.

Ujenzi wa bandari hiyo, utakaochukua miezi 36 kukamilika, ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika ziara aliyioifanya hivi karibuni mkoani humo.

Ujenzi wa bandari hiyo yenye thamani ya Sh. bilioni 266 utakapokamilika, itakuwa na uwezo wa kutengeneza ajira zipatazo 30,000 zikiwanufaisha wavuvi, wakulima wa mwani na wafanyabiashara wengine wa ndani na nje ya nchi.

Hii inaelezwa kuwa ni bandari ya kwanza kubwa ya uvuvi katika ukanda wa pwani ya Tanzania, lakini kutokana na ukubwa wa ukanda huo, haitatosheleza mahitaji.

Alizungumza katika hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa bandari hiyo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alibainisha kuwa bandari hiyo itakuwa



Meli ya uvuvi

na uwezo wa kuhudumia meli kubwa zipatazo kumi kwa wakati mmoja.

Aidha, bandari hiyo itakuwa na chumba cha kuhifadhi samaki chenye uwezo wa kuhifadhi zaidi ya tani 1,000 za mazao hayo ya maji kwa wakati mmoja.

“Pia tutakuwa na huduma za kuchakata samaki ambapo tutawawezesha wavuvi wadogo kuongeza tija kutoka kuvua kilo moja ya samaki hadi kuvua zaidi ya kilo 100 kwa siku wakati akina mama wakizalisha zaidi ya tani 10,000 za mwani kutoka kiasi cha tani 4,000 wanachozalisha sasa,” alisema Ulega.

Mafanikio ya Tasac

Akizungumzia mafanikio ya shirika hilo katika mkutano ya wahariri hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Mlali alibainisha kuwa licha ya uchanga wake, Tasac imeweza kuongeza mchango wake katika pato ya serikali hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 43 mwaka 2021/22 kutoka kiasi cha bilioni 9.1 mwaka 2018/19.

Aidha, Tasac imeweza kuongeza idadi ya meli za kigeni zilizokaguliwa nchini kutoka meli saba mwaka 2018 hadi meli 39 mwaka jana, ikionesha kuongezeka kwa uwezo wa wakaguzi wa meli nchini kwa kuzingatia mahitaji ya kimataifa.

Kwa upande wa leseni za vyombo vidogo, Tasac imeongeza idadi ya leseni zilizotolewa kutoka 2,008 mwaka 2018 hadi leseni 6,366 mwaka jana.

Tangazo



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Wakili Mtanzania pekee ICC anayetamani Katiba mpya

Revocatus Kuuli ambaye aliwahi kuwa Wakili wa Serikali Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, ndiye Mtanzania pekee wakili katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) iliyoko The Hague, Uholanzi, anaeleza mengi kuhusu mahakama hiyo kama alivyohojiwa na mwandishi wa Pambazuko, Tryruckia Mfinanga.

xxxxx

Swali: Hebu tueleze malengo hasa ya kuwepo kwa ICC, inavyofanya kazi na Tanzania inafaidika nini kuwa mwanachama wa ICC? Je, manufaa binafsi ya wakili wake ni yapi?

Jibu: Tanzania ni moja ya nchi zinazounda ICC kupitia sheria iliyoanzisha ICC, yaani Rome Statute, na nchi wanachama ndio zenye wajibu wa kutoa michango ya kuendesha mahakama hiyo, ingawa taasisi zingine zikiwamo Umoja wa Mataifa (UN) na Jumuiya ya Ulaya (EU) nazo huchangia fedha kwa kiasi kikubwa.

Uamuzi wa kuanzisha ICC ilikuwa ni kuhakikisha wahalifu wa makosa ya kivita, uvamizi wa Nchi moja Kwa nchi nyingine, mauaji wa kimbari, uhamishaji wa halaiki ya watu Kwa mabavu, wapiganaji matumizi ya watoto vitani, mauaji ya raia katika mapigano, hawakwepi mkono wa sheria.

Na kwamba hawapati kinga ya kushtakiwa kwa uhalifu wao (impunity) na kama wahalifu hao wana Kinga katika nchi zao, basi kinga hiyo haitamzuia Mwendesha Mashtaka wa ICC kuwafungulia mashtaka.

Tanzania kuwa mwanachama ICC kunaifanya nchi kuwa na msimamo wa kupiga vita uhalifu wa kivita, mauaji ya kimbari, uvamizi wa nchi moja Kwa nchi nyingine na makosa mengine yote yaliyomo katika Sheria ya Roma, lakini pia hii ni hatua kubwa ya maendeleo ya diplomasia ya nchi yetu Kwa kuwa nchi ni sehemu ya jumuiya ya kimataifa.



Kuuli

Faida zangu binafsi nikiwa wakili wa ICC ni kwamba kitaaluma sasa ni wakili wa kimataifa, nina uwezo wa kumtetea mshtakiwa au muhanga katika mahakama ya kimataifa.

Swali: Unaweza kutueleza kinagaubaga Kwanini baadhi ya viongozi wa mataifa makubwa na tajiri, wanapokuwa watuhumiwa ICC, hawakamatiki?

Jibu: Kimsingi hakuna mtuhumiwa au mshtakiwa ambaye hakamatiki na ICC, mahakama ile ina mikono mirefu ndio sababu hata wanaojiwekea kinga inawakamata, ni majuzi tu mahakama imetoa amri ya kuwakamata wakubwa fulani kule Russia kwa tuhuma za uhalifu kule Ukraine.

Lakini pia kulikuwa na amri ya kumkamata aliyekuwa kiongozi wa Sudan, Omar al-Bashir kwa tuhuma za uhalifu nchini Sudan, nadhani hii ni mifano mizuri, watuhumiwa hawa walizuru Afrika Kusini kwa nyakati tofauti kukiwa na amri hizo.

Mahakama Afrika Kusini ilitoa amri ya kumkamata Al-Bashir baadaye serikali ya nchi hiyo ikamsaidia kuondoka kukwepa mkono wa sheria nadhani ndivyo ilivyotokea kwa Vladimir Putin kiongozi

Mahojiano

Wakili Mtanzania pekee ICC

Inatoka Uk. 15

wa Rusia na hili siyo tatizo la ICC, ni tatizo la nchi wanachama kutotimiza wajibu wao wa kuisaidia Mahakama yao.

Nchi wanachama zikitimiza wajibu hakuna mkubwa wala mdogo, watuhumiwa wote watakatamwa. Ni wajibu wa nchi wanachama kuheshimu na kutekeleza mikataba ya kimataifa ambayo nchi imeiridhia.

Swali: Wewe ni wakili wa Mahakama ya Afrika, na mahakama kuu za hapa Tanzania, tueze ICC huchukua hatua gani pale nchi mwanachama inapokataa ama Inaposhindwa kutoa ushirikiano kumkamata mtuhumiwa ?

Jibu: Kimsingi, mikataba mingi ya kimataifa hutekelezwa kwa uhusiano wa kidiplomasia zaidi badala ya kumuadhibu mwanachama anayeshindwa kutekeleza jambo walilokubaliana.

Kwa mfano, mwanachama hajatoa mchango wa uanachama, badala ya kulipa mchango na faini anaweza kukumbushwa kulipa au hata kufutiwa deni ili kuimarisha uhusiano na hali iko hivyo pia kwa wanachama wa ICC ambao hushindwa kuwakamata washtakiwa marafiki hukumbushwa kutimiza wajibu wao.

Swali: Ikiwa Mtanzania atakuwa na kesi ICC, anaweza kutetewa na wakili yeyote ?

Jibu: Ni kweli, mshtakiwa au muhanga mwenye kesi ICC anaweza kutetewa na wakili yeyote, lakini kama ilivyo katika mahakama zingine, taaluma ya mawakili ni taaluma adhimu na ambayo ina uangalizi madhubuti sana, kwa hiyo katika ICC, lazima ufanyiwe upekuzi (vetting) kabla ya kusajiliwa na ICC.

Orodha ya mawakili ICC ni mali ya msajili wa mahakama hiyo, na Kila wakili ana wasifu katika orodha hiyo. orodha hiyo hutolewa kwa wahanga na washtakiwa ili wachague mawakili wanaokidhi mahitaji yao.

Lakini pia ni lazima kwa wakili kujua miongozo na kanuni mbalimbali za



Kuuli

mahakama hiyo, unaweza kuona jinsi wakili mwingine ambaye hajasajiliwa na ICC anavyoweza kupata ugumu wa kufanya kazi ICC.

Kwa kuwa kila mshtakiwa au muhanga ana haki ya kupata utetezi kwa kanuni za mahakama hata kama hana fedha za kumlipa wakili, mahakama imempa mamlaka msajili kumteua wakili yeyote katika orodha ya mawakili wake kumtetea muhanga au mshtakiwa na wakili huyo hulipwa na Mahakama yenyewe.

Mahakama pia huandaa mafunzo kwa mawakili wake Kama niliyoshiriki mwezi Septemba huko The Hague, na kimsingi wakili ambaye hajasajiliwa ICC awezi kuwa na viwango vya ICC.

Swali: Vipi ICC kuna gharama zozote za ada kuwa wakili?

Jibu: Jopo la usaili wa waomba Uwakili wa ICC wakijiridhisha kuwa muombaji ana sifa za kuorodheshwa, kawaida humpatia hati ya kuorodheshwa na mahakama na hakuna malipo.

Isipokuwa kuna ada ya Euro 150 (Sh. 400,000) kuwa mwanachama wa Chama cha Mawakili wa ICC. Uanachama katika chama hiki si wa lazima ingawa Mimi ni mwanachama, mazungumzo yanaendelea kati ya mahakama na chama kuwzesha uanachama kuwa suala la lazima.

Endelea Uk. 17

Wakili Mtanzania pekee ICC

Inatoka Uk. 16

Swali: ICC imekuwa ikihusika zaidi na kesi kubwa za mauaji na unyanyasaji dhidi ya binadamu, unawashauri nini viongozi wetu kuhusu madhara ya ukiukaji wa haki za binadamu? Nini ushauri wako kwa viongozi wetu na hasa kuhusu utawala bora ?

Jibu: Utawala bora ndiyo msingi wa haki na kinyume cha utawala bora ndio udikteta, uchu wa madaraka, ukiukaji wa haki za binadamu, ufidadi, kukosekana uwazi na udanganyifu katika uchaguzi, mambo ambayo ni vyanzo vikubwa vya vurugu, mapigano, na mauaji ya raia wasio na hatia.

Hakuna ubishi kuwa mamilioni ya watu wameuawa au kukimbia makazi au nchi zao kunusuru maisha kutokana na kukiukwa kwa misingi ya utawala bora.

Ushauri wangu ni kwamba viongozi na watawala wazingatie misingi ya utawala bora na kwa kufanya hivyo wataongoza watu wao kwa haki na kuepusha kuwamimbia Wananchi mvua za risasi ama kuwafunga kwa mashauri ya uongo kila kuchapo.

Swali: Ukipewa nafasi moja tu ya kubadili baadhi ya sheria za Tanzania, ni ipi utaamuru iondoke na kwa nini ?

Jibu: Kama una maana ya sheria za kawaida nitabadili haraka Sheria ya Uchaguzi naona bado inafanya sana haki za kisiasa mathalan, haki ya kuchagua na kuchaguliwa bila kujali kama ni mwanachama wa chama fulani au la.

Katika mabadiliko hayo, naamini Tanzania tutakuwa na uwezo wa kupinga mahakamani matokeo ya kura za rais, kuruhusu mgombea binafsi na kubwa zaidi tutakuwa na tume huru ya uchaguzi.

Lakini nadhani badala ya kufikiria sheria moja moja muhimu zaidi ni kuandika Katiba mpya itakayozingatia misingi ya utawala bora na kuweka wajibu kwa watakoaisimamia, tukiandika Katiba mpya itasaidia kuboresha zile zinazokinzana na Katiba.

Swali: Wakili umeacha kazi serikaini



Chumba cha kuhifadhi kumbukumbu za ushahidi katika Mahakama ya ICC, The Hague.

ambako ulikuwa na cheo kikubwa, nini matarajio yako Sasa Kama Wakili wa Kimataifa wa kujitegemea ?

Jibu: Niliacha kazi Kwa hiari ili nitafute fursa nyingine, na kwa kweli naona Mungu ananifungulia fursa, matarajio yangu makubwa wakati naacha kazi yalikuwa kutafuta fursa ambazo hazitafunga fikra zangu.

Nilipenda kufanya kazi na asasi za kiraia au taasisi za kimataifa hiyo ndio kiu yangu.

Swali: Je, ikitokea umepata fursa ya kurejea kufanya kazi serikalini, uko radhi?

Jibu: Ikitokea nikapata kazi nyingine ya serikali tofauti na nilizowahi kutumikia, naweza kutoa mchango wangu huko.

Swali: Baada ya kupata mafunzo ya namna ya kutumika ndani ya ICC, nini hasa unaweza kujivunia?

Jibu: Weledi wangu umeongezeka hususan katika haki jinai ya kimataifa na sheria za kimataifa kwa ujumla, mafanikio niliyopata si haba kwa kuwa ili uwe wakili ICC lazima uwe umefanya kazi ya uwakili katika nchi iliyokusajili kuwa wakili kwa miaka isiyopungua kumi au uwe profesa wa sheria na uthibitishie unafahamu vyema sheria za kimataifa, haki za binadamu na sheria zinazowalinda raia katika vita au mapigano na itifaki zake.

Mafanikio haya yameniwzesha kudahiriwa kufanya shahada ya uzamivu katika sheria za kimataifa na mikataba ya Kimataifa yaani (PhD in International Law and Treaty Law) katika Chuo Kikuu cha Euclid, Gambia.

Riwaya

Tetemeko la ndumba - 4

Mtunzi: Innocent N. ZAGALLO

ALIPOFIKA Magomeni alikodi teksi aliyompeleka katika gesti moja ambako alichukua chumba na kuanza kupanga hatua moja baada ya nyingine katika kazi iliyomkaabili, kazi ngumu lakini aliyoamimi kuwa isingemshinda.

Jumapili asubuhi, hii ikiwa ni siku ya pili baada ya kuingia jijini Dar es Salaam, Mzee Songoro aliamka mapema, akaoga na kupata stafutahi katika mgahawa uliokuwa jirani na gesti hiyo.

Mazingira ya hali ya hewa ya jiji hilo yalimpa shida lakini alivumilia. Japo ndiyo kwanza ilikuwa ni saa 1.30 asubuhi, hata hivyo alihisi joto kali mwilini tofauti na hali ya hewa ya Kigoma. Alikunywa chai kwa kuwa tu lililazimu afanye hivyo kutokana na njaa kali iliyomsakama tumboni.

Alipomaliza alitoka huku akijifuta jasho kwa lesa yake chakavu. Akaliacha eneo hilo kwa mwendo wa asteaste huku akiwa na chupa ya maji baridi mkononi na kijibegi chake begani.

Mfukoni alikuwa na shilingi 250,000 tu ambazo alizichukulia kuwa ni kiasi kidogo cha pesa kisichostahili kujivunia kutokana na majukumu mengi na muhimu yaliyokuwa mbele yake. Lakini pamoja na hayo, bado aliamini kuwa akiwa makini katika matumizi, fedha hizo zitasosha kwa jambo lolote alilodhamiria kulifanya.

Alipanga kuanza operesheni yake kwa kuzungukia magereza ya Keko, Ukonga na Segerea. Kama Shaka hatakuwa katika magereza hayo, angeitumia siku hiyo kufanya utafiti zaidi, ajue gereza lililomhifadhi na kumfuata hukohuko aliko hata kama ni mkoa mwingine.

Alianzia Segerea. Jibu alilolipata huko ni kwamba hakukuwa na mfungwa mwenye jina la Shaka, wala kwa wiki nzima iliyopita hawajawahi kumpokea mtu mwenye tuhuma nzito kama alizowaeleza.

Akaenda Ukonga.



Uganga

Patupu!

Ni katika gereza la Keko ndipo alipopata jibu zuri. Askari mmoja alimwambia kuwa majuzi walimpokea jambazi sugu mwenye jina hilo. Likawa ni jibu lililomtia faraja mzee Songoro. Papohapo akatwaa mzizi ndani ya mfuko wa shati na kuutia mdomoni. Akaanza kuutafuna taratibu bila ya kuumeza. Na alikuwa na sababu ya kufanya hivyo.

Mzizi huo ulikuwa na nguvu za ajabu. Mtu yeyote akiutia mdomoni, na kuutafuna huku akizungumza na mtu mwingine, basi chochote atakachokisema huyo mtumiaji mzizi kitakubaliwa na msikilizaji.

Watumiaji wengi wa mzizi huo ni wale wanaokwenda mahali kutafuta ajira, wakware na wenye kesi mahakamani. Mzee Songoro alikuwa ni miongoni mwa watu hao. Na alipoutia mzizi huo kinywani, matumaini ya mafanikio yakazidi kumjaa.

Jumapili hiyo ilikuwa ni siku maalumu kwa ndugu, jamaa na marafiki kuruhusiwa kuonana na wafungwa. Na nje ya gereza hilo kulikuwa na umati mkubwa wa watu waliokuja kwa madhumuni hayo ya kuonana na ndugu zao ambao baadhi walikuwa wakitumikia vifungo na baadhi walikuwa rumande wakisubiri hukumu za kesi zilizowakaabili.

Itaendelea wiki ijayo...

Walilia Gaza

Wanasoka waunga mkono Palestina

Na Mwandishi WETU

WANASOKA maarufu duniani wameunga mkono Palestina hadharani huku wakionesha mshikamano wao na kulaani mashambulizi ya Israel thidi ya taifa hilo.

Taarifa iliyokusanywa na Shirika la TRT, inaeleza kuwa mchezaji wa zamani wa Arsenal, Mesut Ozil amekuwa mmoja wa nyota waliozungumzia hali hiyo huku wanasoka wengine wakitumia mitandao yao ya kijamii kuiunga mkono Palestina.

Wachezaji mbalimbali wametumia mitandao ya Facebook, Instagram na X, kuonyesha mshikamano wao kwa Palestina.

“Naombea ubinadamu. Naombea amani. Watu wasio na hatia na hasa watoto wasio na hatia wanapoteza maisha yao katika vita hivi. Inavunja moyo na kuhuzunisha. TAFADHALI ACHA VITA!!!”. Aliandika kwenye Ozil katika ukurasa wake wa mtandao wa X.

Mesut Ozil amekuwa akizungumzia suala la Palestina mara kwa mara.

Wachezaji wa Algeria akiwemo Riyad Mahrez, Saïd Benrahma na Ahmed Touba walishikilia bendera ya Palestina baada ya mechi yao dhidi ya Cape Verde hivi karibuni. Mabingwa hao wa Afcon 2019, waliishinda Cape Verde 5-1 katika mechi ya kirafiki iliyochezwa alhamisi Oktoba 12.

Huku hayo yakiiriri, mchezaji wa Algeria Youcef Atal ametishiwa na Meya wa Jiji la Nice, Christian Estrosi aliyetumia mtandao wa X, kulaani maandiko ya mwanasoka huyo yalionekana kuunga mkono Palestina.

“Natarajia Youcef Atal, kuomba msamaha na kulaani magaidi wa Hamas kwa kukubali kutumiwa vibaya. Ikiwa hatofanya hivyo, hawezi kuwa tena na nafasi ya kuiwakilisha timu yetu ya Nice, ameanzika meka huyo.

Mbali na hayo, mabingwa wa Ligi ya Mabingwa wa Soka Afrika, Al-Ahly kutoka Misri, ambayo ilibeba taji lake la



11 la Afrika kwa ushindi wa 3-2 dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco, imetoa taarifa kwenye ukurasa wake wa X, ikiandika kuwa pamoja na Palestina.

Mashabiki wa klabu ya soka ya Morocco, Raja CA walishangilia na kuunga mkono Palestina huku wakiinua bendera za Palestina wakati wa mechi wa klabu hiyo iliyopigwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Soka wa Mohammed V mjini Casablanca.

Mashabiki wa timu ya taifa ya soka ya Bolivia nao walinyanyua bendera ya Palestina kwenye mechi kati ya Ecuador na Bolivia.

Wakati huohuo, mashabiki wa timu ya Celtic wameunga mkono kwa kushikilia bendera za Palestina wakati wa mechi ya ligi ya Scotland kati ya Celtic na Kilmarnock huko Celtic Park, Oktoba 7, 2023, mjini Glasgow, Scotland.

Nchini Qatar, wachezaji kutoka timu za Al Gharafa na Al Duhail, wakiwemo mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Algeria Yacine Brahimi, walishikilia bango la kuunga mkono Palestina kabla ya mechi yao ya Kombe La Qatar likiwa limeandikwa, “Palestina, daima na milele katika miyo yetu.”

CHANDA CHEMA...



Mwenyekiti wa Kikundi cha Wajasiriamali Wanawake wa Bunju (BWE), Jacqueline Mkina akionesha zawadi ya ngao aliyokabidhiwa baada ya kuibuka kidedea kwa kuwa kiongozi bora wa kikundi cha wanawake Dar es Salaam. Sherehe ya kuwaenzi wanawake wa Dar es Salaam ilifanyika Ubungo Plaza, Jumamosi – Oktoba 14, ikienda sambamba na maadhimisho ya kukumbuka ya maisha ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. (Picha kwa hisani ya BWE)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

